AckySHINE.com

# Je, kwa nini akina mama wajawazito hawatakiwi kunywa pombe?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Wanawake wajawazito ambao hunywa pombe au kuvuta sigara wanahatarisha afya na maisha ya mtoto aliye tumboni. Mtoto aliye tumboni hurutubishwa kupitia damu ya mama. Kama mama atavuta sigara au kunywa pombe, sumu illiyopo katika sigara au pombe inapoingia kwenye damu yake itamfikia mtoto pia. Pombe hushambulia moyo uendeleao kukua na ubongo wa mtoto aliye tumboni. Akina mama wanaokunywa kupita kiasi wakiwa wajawazito wanaweza kupata watoto wenye magonjwa ya moyo au mtindio wa akili, kwa sababu chembechembe za ubongo hazikui vizuri. Mara nyingi watoto huzaliwa na upungufu katika mwonekano wa sura. Kwa mtoto pombe ni sumu kali, hata kama ni kwa kiasi kidogo, itamdhuru.

Mama anaekunywa pombe anaweza kuwa hajali au kusahau kujilinda mwili wake na mtoto anayekua. Kama akipata maambukizo ya VVU na mtoto pia anaweza akapata virusi vya UKIMWI. Wanawake wanaovuta sigara wakiwa wajawazito wana uwezekano mkubwa wa kuzaa watoto ambao hufariki ghafla bila sababu ya kueleweka katika mwaka wao wa kwanza wa maisha. Watoto wa akina mama wanaovuta sigara mara nyingi huzaliwa na umbo dogo kuliko wengine kwa sababu watoto walipata chakula kidogo walipokuwa bado tumboni mwa mama zao. Ujumbe upo wazi: Wanawake wanaotaka watoto wenye afya wasivute kabisa sigara wala kunywa pombe wakiwa wajawazito.